“Dashboard” ni mfumo unaotumika kufanya tathmini ya kiwango cha utawala bora katika mipango ya uhifadhi wa misitu kwenye jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu Tanzania. Mfumo huu utatumika kuchunguza yafuatayo;

Kiwango cha uwazi katika shughuli za usimamizi wa misitu na matumizi ya fedha,

Ushirikishwaji wa jamii katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na misitu wanayohifadhi

Ushirikishwaji wa jamii katika kupanga matumizi ya fedha zitokanazo na misitu wanayohifadhi.

Kiwango cha usawa katika kugawana faida zitokanazo na usimamizi shirikishi wa misitu

Utawala wa sheria

Jinsi ngazi za wilaya zinavyounga mkono usimamizi shirikishi wa misitu.

Matokeo ya mfumo huu yatasaidia kulinganisha jamii moja na nyingine au wilaya moja hadi nyingine katika masuala ya utawala bora ndani ya mipango ya usimamizi wa misitu na kuzifanya jamii kutambua matatizo au mapungufu mbalimbali yaliyopo na kutafuta mbinu za kuboresha hali hiyo.

Nani atafanya tathmini hii?

Tathmini hii itafanywa na WANAMJUMITA toka kwenye vijiji husika ambao si wajumbe toka kwenye serikali ya kijiji au wajumbe wa kamati ya maliasili/msitu ya kijiji. Watathmini hao watachaguliwa kwenye mikutano mikuu ya mitandao chini ya uangalizi wa mratibu wa kanda au msaidizi wake. Watu wawili watachaguliwa kutoka kila kijiji kilichoteuliwa ndani ya mkutano mkuu wa mtandao, na kisha watathmini hao watapatiwa mafunzo na mratibu wa kanda husika ya jinsi ya kufanya mijadala hiyo na kukusanya takwimu. Baada ya kupata mafunzo na kufanyiwa majaribio, watathmini watakuwa tayari kwa kukusanya takwimu.

Utambulisho kwa uongozi wa kijiji

Baada ya kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kufanya mijadala na kukusanya takwimu, mtathmini atatakiwa kuchukua barua ya utambulisho toka kwa mratibu wa kanda inayoelezea lengo la zoezi zima pamoja na kumtambulisha yeye kwa uongozi wa serikali ya kijiji. Baada ya kupewa ruhusa na uongozi wa serikali ya kijiji ya kuendelea, mthathmini ataelezea kwamba atahitaji kufanya majadiliano na Mwenyekiti na mtendaji wa kijiji pamoja na Mwenyekiti na katibu wa kamati ya msitu wa kijiji katika ofisi ya serikali ya kijiji, atapenda pia kupata nyaraka mbalimbali zilizopo kama mpango wa usimamizi wa msitu, sheria ndogo za msitu, daftari la doria, daftari la faini, takwimu za mapato na matumizi na nyaraka zinginezo kama muhtasari wa vikao n.k. Na mwisho atafanya majadiliano na kikundi cha watu wasiozidi kumi kama taratibu za kuwachagua zilivyoainishwa hapo chini.

Jinsi ya kuchagua washiriki wa mjadala

Tafadhili unaombwa kuchagua watu kumi (10) kijijini watakaoshiriki mjadala huu.

Hakikisha kwamba, washiriki wa mjadala huu si wajumbe katika Kamati ya Maliasili/Msitu ya Kijiji au Serikali ya Kijiji.

Hakikisha kwamba kila kitongoji kinatoa wawakilishi wake watakaohudhuria mjadala huu.

Wajumbe watakoachaguliwa lazima wawe na uelewa kuhusu masuala ya uhifadhi wa misitu/maliasili kijijini (kwa mfano; wafunga nyuki, wanaohifadhi misitu yao binafsi, na wengineo)

Wajumbe watakoachaguliwa lazima watoke katika nyumba (familia) tofauti, yaani nyumba moja itoe mtu mmoja tu.

Uchaguzi wa wajumbe lazima uzingatie jinsia zote yaani kuwe na wanawake 5 na wanaume 5

Andaa sehemu kwa ajili ya kufanyia mkutano huo

Viongozi wa vijiji kama mwenyekiti wa kijiji na mtendaji hawataruhusiwa kuhudhuria mjadala huu bali watafanya mahojiano na mthathmini kwenye ofisi ya serikali ya kijiji.

Kanuni za uendeshaji mjadala au mambo ya kuzingatia wakati unapoendesha mjadala

Elezea na fafania lengo la mjadala huo kwa ufasaha zaidi na hakikisha wajumbe wanakuelewa vizuri kabla haujaendelea

Tumia lugha inayoeleweka kwa kila mjumbe, kama wajumbe wengi hawaelewi Kiswahili basi fafania swali kwa kutumia lugha ya asili iliyozoeleka.

Epuka kutumia lugha za kitaalamu pale inapowezekana, endapo kuna umuhimu wa kutumia neno hilo basi hakikisha unalitolea ufafanuzi zaidi na wajumbe wanalielewa vizuri

Elezea kila swali kwa ufasaha na litolee ufafanuzi

Tengeneza mazingira ya kiurafiki zaidi kati yako na wahojiwa ili kupata majibu yenye ukweli.

Anza mjadala kwa maongezi ya kawaida kwa mfano; ulizia hali ya hewa ikoje, mavuno ya mazao mwaka huu yakoje n.k.

Kuwa makini sana na maswali yanayogusa hisia za wajumbe moja kwa moja, kama kuna swali la aina hiyo jaribu kuliuliza kwa njia nzuri na ya kirafiki zaidi.

Epuka kutumia maneno makali na ya kiubaguzi

Endapo mjumbe anaonekana kutoka nje ya mada inayozungumziwa, tafuta kauli nzuri itakayomrudisha kwenye mada bila kumfanya ajisikie vibaya

Epuka kuandika jibu la mtu mmoja, majibu yote yanayotolewa ni lazima yakubaliwe na washiriki wote kabla ya kuandikwa kwenye dodoso.

Hakikisha kila mshiriki anatoa mawazo yake na epuka mtu mmoja kutawala mjadala wote.

Jinsi ya kuwasilisha taarifa zilizokusanywa

Baada ya kukusanya taarifa hizi, tafadhali weka nakala moja iliyojazwa kikamilifu kwenye bahasha kubwa iliyoandaliwa na kuwekwa anuani ya posta na Mratibu wa kanda. Wasiliana na Mratibu wa kanda na umtumie nakala hiyo kwa njia ya posta. Nenda kwenye ofisi ya posta iliyo karibu na eneo unaloishi na

utume nakala hiyo. Nakala ya pili ikabidhiwe kwenye uongozi wa serikali ya kijiji kwa ajili ya kumbukumbu za ofisi na nakala ya tatu unatakiwa kubaki nayo ili itakapotokea kwamba taarifa uliyotuma haikufika basi nakala iliyobaki itumike.

Malipo kwa ajili ya chakula kwa washiriki

Kutakuwa na malipo kwa ajili ya chakula kwa watu wote watakaoshiriki zoezi hili, washiriki hao ni watu kumi (10) watakaoshiriki kwenye mjadala wa kikundi, viongozi toka serikali ya kijiji na Kamati ya maliasili 4 (Mwenyekiti wa kijiji, Mtendaji, Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya maliasili) na watathmini 2. Kila mtu atalipwa gharama ya shilingi 3,000/= za kitanzania kama gharama za chakula, maji na soda. Pesa hiyo atapewa mtathmini siku atakapokabidhiwa dodoso.

Kila Mtathmini atalipwa shilingi elfu kumi (10,000/=) kama malipo ya kufanya zoezi la kukusanya takwimu hizo. Zoezi hili linategemewa kufanyika kwa muda wa siku moja. Malipo kwa mtathmini yatalipwa pale atakapokabidhiwa dodoso. Ni wajibu wa kila mtathmini kuhakikisha kwamba dodoso lililojazwa linamfikia Mratibu wa kanda kwa muda unaotakiwa.

Urudishwaji wa matokeo ya taarifa zilizokusanywa kwa wananchi

Taarifa toka kwenye dodoso lililojazwa zitafikishwa makao makuu ya ofisi ya MJUMITA na mratibu wa kanda kwa njia ya kuziingiza kwenye “database” iliyoandaliwa na Afisa tekinolojia wa mradi. Takwimu hizo zitatolewa kwenye “database” na kufanyiwa uchambuzi na mwisho taarifa kamili itaandaliwa ikionyesha matokeo ya utawala bora kwa katika kila kijiji. Matokeo ya kila kijiji yatawasilishwa kwenye vijiji husika kwenye mikutano mikuu ya kijiji na jamii itapata fursa ya kujadili hali hiyo katika mkutano huo. Endapo jamii itaonyesha nia ya kufanya mabadiliko kwenye baadhi ya mambo basi utaratibu utapangwa wa jinsi ya kusaidia kutatua tatizo au mapungufu hayo.

Maelekezo kwa kila kipengele kilichopo kwenye dodoso

(Tafadhali tumia dodoso lililoambatanishwa kwenye mwongozo huu, hakikisha unajaza nakala tatu(3) za dodoso; Ofisi ya kanda nakala 1; Ofisi ya serikali ya kijiji nakala 1; Mtathmini nakala 1)

Tafadhali unaombwa kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye sanduku la maelekezo kwa kila kipengele au maelekezo yaliyopo kwenye swali yenye mwandiko wa mlalo na pia ufuate kama maelekezo hayo yatakavyokuagiza. Maelekezo hayo ni kwa ajili ya kumpa mtathmini maelezo ya ziada na hayatakiwi kusomwa kwa wajumbe wa mjadala

Sehemu ya kwanza

Sehemu ya kwanza kwenye dodoso ina lengo la kumtambulisha mtathmini, kufahamu idadi ya watu waliopo kijijini, kufahamu ukubwa wa eneo la msitu wa hifadhi ya kijiji na eneo la msitu lililo nje ya msitu wa kijiji. Pamoja na kufahamu muda unaotumika tangu mpango wa usimamizi wa msitu na sheria ndogo za msitu zinapofikishwa wilayani mpaka kupitishwa. Kipengele hiki kitajazwa kwa msaada wa viongozi wa serikali ya kijiji. Upatikanaji wa nyaraka za mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na sheria ndogo za msitu za kijiji zitakusaidia kujaza kipengele hicho. Utatakiwa kujaza kipengele A au B kutegemeana na aina ya usimamizi shirikishi wa msitu unaofanywa na kijiji husika. Kipengele A kitajazwa tu endapo kijiji husika kinatekeleza mpango wa uhifadhi shirikishi msitu wa hifadhi wa kijiji; kipengele B kitajazwa endapo kijiji kinatekeleza mpango wa uhifadhi shirikishi wa pamoja yani kati ya halmashauri ya kijiji na serikali kuu; na endapo kijiji kinatekeleza mipango yote miwili yaani mpango shirikishi msitu wa hifadhi wa kijiji na ule wa pamoja kati ya halmashauri ya kijiji na serikali kuu basi vipengele vyote viwili yaani A na B lazima vijazwe.

Sehemu ya pili

Sehemu hii ina lengo la kufahamu juhudi mbalimbali zinazofanywa na ngazi ya misitu wilaya na vyombo vya usalama kama polisi katika kuunga mkono juhudi za kijiji katika harakati za kutekeleza mipango ya uhifadhi shirikishi wa jamii. Maswali mbalimbali yanayopima utendaji kazi wa mamlaka hizo mbili

yameandaliwa ili yaulizwe kwa Mwenyekiti na mtendaji wa kijiji pamoja na katibu na mwenyekiti wa kamati ya maliasili ya kijiji. Tafadhali tembelea ofisi ya serikali ya kijiji ili uonane na viongozi hao na kufanya mahojiano nao kwa kufuata muongozo wa maswali ya kipengele cha pili.

Sehemu ya tatu

Kipengele hiki kina lengo la kutaka kufahamu kama kijiji kina utaratibu wa kutunza takwimu mbalimbali za shughuli zinazofanyika kijiji na hasa zinazohusu mipango ya uhifadhi wa misitu kijijini. Vile vile kufahamu mipango mbalimbali iliyopo kijiji inayohusu usimamizi wa misitu na jinsi inavyotekelezwa kwa kuzingatia utekelezaji wa sheria zilizowekwa katika kusimamia misitu hiyo. Tafadhali omba nyaraka mbalimbali toka kwenye serikali ya kijiji na katibu wa kamati ya maliasili kwa ajili ya kupata uhakika wa majibu ya taarifa ya maswali yaliyoandaliwa katika kipengele hicho.

Omba nyaraka ya sheria ndogo za misitu, mpango wa usimamizi wa misitu kijijini, takwimu za doria, mapato na matumizi yatoanayo na rasilimali za misitu na mihutasari ya vikao toka kamati ya maliasili na serikali ya kijiji. Hakikisha kwamba kipengele hiki kinajazwa kwa umakini kwa kuangalia majibu ya maswali ya kila kipengele toka kwenye nyaraka husika na wala siyo kuuliza maswali kwa wahusika. Kama nyaraka hizo hazikupatikana, utatakiwa kujibu swali la kwanza katika kipengele hicho na utoe sababu za kukosekana kwa nyaraka hizo na uende kwenye kipengele kinachofuata.

Sehemu ya nne

Maswali ya kipengele hiki yameandaliwa kwa ajili ya kupata taarifa kutoka kwenye kikundi cha wanajamii hapa kijiji kwa njia ya mjadala. Majibu toka kwenye maswali hayo yatatuwezesha kufahamu jinsi jamii husika inavyoshirikishwa katika shughuli za usimamizi wa misitu kijijini; wananchi wanavyoshiriki kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu rasilimali za misitu, mawasiliano kati yao na uongozi wa kijiji pamoja na kuelewa kama kuna uwazi katika mipango ya pesa na kwenye nyaraka mbalimbali kijijini.

Tafadhali elezea kwa ufasaha lengo la zoezi hili kama lilivyoelezwa kwenye sehemu ya utangulizi. Waeleze kwamba ni ruksa kuuliza au kutaka maelezo ya ziada kama kuna swali halijaeleweka vizuri; majibu yote yatapelewa uzito sawa; hakuna malipo au fidia itakayotolewa kwa mtu yeyote atakayeshiriki katika mjadala huu bali ni kazi ya kujitolea; majina ya walioshiriki yatachukuliwa kama kumbukumbu ya ofisi ya MJUMITA na wala hayatatolewa kwa mtu mwingine yeyote na mwisho zoezi hili halina lengo la kunyoosheana vidole kwamba nani amesema nini nani ametenda nini bali kutafuta njia ya kuboresha kiwango cha utawala bora katika kijiji chenu.

Annex iii

Guideline for returning dashboard results

KIONGOZI KWA MTUMIAJI WA KURUDISHA MATOKEO YA UTAFFITI WA UFUATILIAJI UTAWALA BORA KATIKA MISITU

1.0 Utangulizi

Mwongozo huu umeandaliwa baada ya wafanyakazi wa Mradi kufanya ziara ya majaribio ya kurejesha matokeo ya zoezi la ufuatiliaji utawala bora katika vijiji vya vugiri na bagamoyo katika wilaya ya Korogwe, Kwefingo na Milungui katika wilaya ya Lushoto na katika kijiji cha Kipangenge katika wilaya ya Kibaha. Mwongozo huu umeandaliwa ili kuwasaidia wanaMJUMITA kufahamu taratibu mbalimbali zinazotumika kurejesha matokeo ya utafiti wa kufuatilia utawala bora katika vijiji vinavyoshiriki katika usimamizi shirikishi wa misitu Tanzania. Mfumo wa kufuatilia utawala bora umeanzishwa kwa lengo la kuzisaidia jamii ziishizo pembezoni mwa misitu kuibua matatizo mbalimbali ya kiutawala yaliyopo kwenye mipango yao ya usimamizi wa misitu na hivyo kuchochea mabadiliko.

Zoezil hili linafanywa na wanaMJUMITA waliopewa mafunzo ya jinsi ya kukusanya takwimu hizo na kuzifikisha kwenye ofisi za kanda za MJUMITA. Watathmini wawili huchaguliwa kwenye mkutano mkuu wa mtandao chini ya uangalizi wa mratibu wa kanda au msaidizi wake kwa kuzingatia sifa zifuatazo; Ni lazima wawe ni wanachama wa MJUMITA katika kijiji husika, wasiwe wajumbe wa kamati ya maliasili au serikali ya kijiji, wajue kusoma na kuandika vizuri na mwisho jinsia lazima izingatiwe . Takwimu hizi zinakusanywa toka kwa viongozi wa serikali ya kijiji na kamati ya maliasili, nakala zenye takwimu na taarifa mbalimbali zilizopo kijijini na kwenye kikundi cha wananchi wasiozidi 15 ambao si wajumbe wa kamati ya maliasili wala serikali ya kijiji. Takwimu hizo zitafanyiwa uchambuzi yakinifu katika makao makuu ya ofisi ya MJUMITA na matokeo yake hurudishwa kwa watathmini. Watathmini watawasilisha matokeo hayo kwenye uongozi wa kijiji (kamati ya maliasili na wajumbe wa halmashauri ya kijiji) na mwisho kwa wananchi kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Matokeo ya zoezi hili hutoa fursa kwa wananchi kutambua matatizo yaliyopo kijijini kwao, kubaini vikwazo vyake na mwisho kuyatafutia ufumbuzi.

2.0 UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UFUATILIAJI UTAWALA KATIKA NGAZI YA MTANDAO

Matokeo ya vijiji vilivyoshiriki kwenye zoezi la ufuatiliaji utawala bora kwenye kila mtandao wa MJUMITA yatawasilishwa na Mratibu wa kanda kwenye mkutano wa mtandao utakaojumuisha watathmini wa vijiji vyote vilivyofanya zoezi la ufuatiliaji utawala bora pamoja na viongozi wa kijiji (1 toka serikali ya kijiji na 1 toka kamati ya maliasili). Mratibu wa kanda atatoa maelekezo ya jinsi ya kurejesha matokeo ya zoezi hilo pamoja na kutoa mwongozo wa mambo yanayotakiwa kufanywa ili kuboresha hali ya utawala bora(Governance best practices). Baada ya kuwasilisha, nakala ya matokeo ya kila kijiji yatatolewa kwa watathmini wa kijiji husika na kupewa maelekezo ya jinsi ya kuwasilisha matokeo hayo kwenye vijiji vyao.

3.0 UWASILISHAJI WA MATOKEO KATIKA NGAZI YA KIJJI

Baada ya kupokea matokeo ya ufuatiliaji utawala bora toka kwa Mratibu, watathmini watauomba uongozi wa serikali ya kijiji kuitisha mkutano wa ndani utakaojumuisha wajumbe wa serikali ya kijiji na wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji. Katika mkutano huu watathmini watapata fursa ya kurejesha matokeo ya zoezi la ufuatiliaji utawala bora yatakayosaidia wajumbe kuibua vikwazo/matatizo yanayosababisha kutofikiwa kwa misingi ya utawala bora na kupendekeza suluhisho kwa ajili ya kuimarisha utawala bora.

3.1 KUWASILISHA MATOKEO YA UTAFFITI KWA VIONGOZI WA KIJJI

Baada ya mwenyekiti kufungua kikao na taratibu zingine za mkutano kufanyika, Mtathmini atakaribishwa kuwasilisha matokeo yaliyopatikana kutokana na zoezi la ufuatiliaji utawala bora kwa kupitia kipengele kimoja kimoja kama ilivyoonyeshwa kwenye nakala ya matokeo(Angalia nakala na. 1 kwenye

kiambatanisho). Ili kuleta mtiririko mzuri utakaoleweka kwa washiriki mtathmini atasoma swali pamoja na jibu lililopatikana toka kwenye utafiti na mwisho atawasilisha mambo yanayotakiwa kufanyika katika kipengele hicho ili kuimarisha utawala bora (Angalia nakala na. 2 kwenye kiambatanisho). Baada ya kumaliza kuwasilisha mtathmini atarudisha nafasi kwa mwenyekiti/mtendaji wa kijiji ambaye ataendesha kikao kwa kutoa fursa kwa wananchi kujadili kama wanakubaliana na matokeo yaliyotolewa au la, baada ya kufikia muafaka washiriki watatakiwa kujadili kwa undani sababu/vikwazo vya kutofikiwa kwa misingi ya utawala bora. Utaratibu huu utatumika kwa kila swali, vikwazo pamoja na suluhisho vitanakiliwa vizuri na Mtendaji wa kijiji, Katibu wa kamati, kiongozi wa mtandao na watathmini. Na mwisho matokeo ya mjadala huu yatawasilishwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji.

3.2 KUWASILISHA MATOKEO KATIKA MKUTANO MKUU WA KIJJI

Viongozi wa kijiji wataitisha mkutano mkuu wa kijiji utakaofanyika baada ya mtathmini kuwasilisha matokeo kwa wajumbe wa serikali ya kijiji na wa kamati ya maliasili.

Baada ya taratibu za kufungua mkutano, mtathmini au kiongozi wa mtandao ataelezea lengo la kufanyika kwa zoezil hilo jinsi takwimu zilivyokusanywa, nani alikusanya takwimu na takwimu zilikusanywa toka makundi gani ya watu. Mtathmini atapewa nafasi ya kuwasilisha matokeo ya ufuatiliaji utawala bora kwa kutumia utaratibu ule ule uliotumika wakati wa kuwasilisha matokeo kwa viongozi (kuwasilisha swali, jibu lililopatikana pamoja na nini kinatakiwa kufanyika ili kufikia misingi ya utawala bora). Baada ya mtathmini kuwasilisha majibu ya maswali yote na misingi ya utawala bora, mtendaji wa kijiji au katibu wa maliasili atasoma vikwazo vilivyoibuliwa na suluhisho lililopendekezwa kwenye mkutano wa serikali ya kijiji na kamati ya maliasili. Utaratibu huo utatumika kusoma maswali yote yaliyoandaliwa kwa ajili ya zoezi hilo, wananchi wataombwa kunakili maswali yao mpaka hapo mtathmini na viongozi wa kijiji watakapomaliza kuwasilisha.

Zoezi la kuwasilisha litakapomalizika, mwenyekiti wa kijiji atawaomba wananchi kujadili kama wanakubaliana na matokeo ya utafiti, vikwazo vilivyotolewa na suluhisho lililopendekezwa kama linaweza kutatua tatizo lililopo.

Wananchi wapewe muda wa kutosha wa kujadili mada husika na mwisho watoe mapendekezo ya jinsi ya kuboresha taarifa hiyo.

4.0 KUFUATILIAJI UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZILIZOKUBALIWA KAMA SULUHISHO LA KUBORESHA UTAWALA

Kipimo cha utekelezaji wa shughuli zilizokubalika kama suluhisho la kuboresha utawala bora katika misitu litafanywa na zoezi lingine la ufuatiliaji utawala bora kila baada ya mwaka. Kwa hiyo Wajumbe wa kamati ya maliasili na serikali ya kijiji wanapaswa kuhakikisha kwamba kile kilichoamuliwa kama ufumbuzi wa matatizo yaliyoibuliwa kimetekelezwa kabla ya kurudia kwa zoezi hili. Vile vile wananchi wana jukumu la kuhakikisha kwamba mapendekezo waliyoyatoa yanatekelezwa kwa wakati kwa kuomba kupewa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa masuala hayo kutoka kwa viongozi wao hasa katika mikutano mikuu ya hadhara na kushinikiza utekelezaji.

APPENDIX 2

MWONGOZO WA SHUGHULI ZINAZOIMARISHA UTAWALA BORA KATIKA VIJJI VINAVYOSHIRIKI KATIKA USIMAMIZI WA MISITU

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia wana MJUMITA na wananchi wengine wanaoishi pembezoni mwa misitu na wanashiriki katika mipango ya uhifadhi wa misitu kuweza kutekeleza shughuli mbalimbali zinazoimarisha utawala bora kwa lengo la kuimarisha usimamizi endelevu wa misitu na kuboresha maisha ya watu wanaotegemea rasilimali za misitu. Mwongozo huu unatoa baadhi ya shughuli au mambo ambayo yakitekelezwa yatapelekea kuimarika kwa utawala bora katika sekta ya misitu

Matokeo ya zoezi la ufuatiliaji utawala bora lilofanywa na Wana MJUMITA la kukusanya taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya utawala katika vijiji vyao yatakimwa/kufanyiwa tathmini kwa kulinganishwa na shughuli zilizoanishwa na hivyo kuonyesha hali halisi ya utawala bora katika kijiji husika. Shughuli zilizopendekezwa kama kipimo cha utawala bora katika vijiji vinavyoshiriki katika usimamizi wa misitu ni kama zifuatazo;-

Mikutano ya kamati ya maliasili

Ili kuimarisha utawala bora katika kijiji ni lazima ihakikishwe kwamba kamati ya maliasili inafanya mikutano 12 au zaidi kwa mwaka. Mikutano hiyo ni muhimu sana katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa rasilimali za misitu kijijini. Mikutano huwapa wanakamati fursa ya kupanga mipango ya utekelezaji wa shughuli zao za kila siku katika kusimamia rasilimali za misitu, kupeana taarifa mbalimbali zinazohusu usimamizi wa rasilimali za misitu, kutambua changamoto zinazowakabili na kutafuta njia bora ya kupambana na changamoto hizo. Vile vile mkutano ni sehemu ambayo wanakamati hupata fursa ya kufanya maamuzi yao kwa sauti ya pamoja juu ya jambo fulani.

Doria zinazofanywa na kamati ya maliasili

Ili kuhakikish kwamba misitu ya kijiji inakuwa katika hali nzuri ambayo ni endelevu, wajumbe wa kamati ya maliasili ya kijiji wanawajibika kufanya doria angalau mara 12 au zaidi kwa mwaka ili kuhakikisha kwamba shughuli zote zilizokatazwa kufanyika ndani ya msitu wa hifadhi wa kijiji hazifanyiki. Na kwa shughuli zilizoruhusiwa kufanyika ndani ya msitu kwa kibali basi zifanyike chini ya uangalizi wa kamati ya maliasili. Wajumbe wa kamati wanashauriwa kupanga doria za kushutukiza ili wahalifu wasipate nafasi ya kujiandaa kutoka kwenye msitu wa kijiji kabla ya kukamatwa. Vile vile wanakamati wanashauriwa kuwa wenye usiri mkubwa pindi wanapopanga siku na wakati wa kwenda kufanya doria ili kuweza kukomesha uhalifu.

Eneo la matumizi endelevu kwa wananchi

Katika kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uhifadhi endelevu wa misitu kijijini ni muhimu kutenga eneo katika msitu wa hifadhi ya kijiji kwa ajili ya matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Zoezi hili linawe kufanyika katika vijiji vinavyohifadhi msitu wa hifadhi wa kijiji kwa msaada wa wataalamu wa misitu. Endapo msitu uliohifadhiwa una lengo la kutunza vyanzo vya maji basi wananchi wanatakiwa kutenga eneo la msitu lililopo nje ya hifadhi hiyo ili kuwezesha uvunaji endelevu wa rasilimali za msitu kufanyika. Kupitia msaada wa wataalamu wa misitu kijiji kitatengeneza mpango wa usimamizi wa msitu utakaobainisha kiwango cha mazao kitakachovunwa kwa mwaka katika eneo hilo na kuonyesha mchakato mzima unaoruhusu uvunaji wa rasilimali hizo. Shughuli yeyote itakayofanyika katika eneo hilo lazima iwe na kibali maalumu kitakachoonyesha aina ya bidhaa inayovunwa, kiwango cha bidhaa inayovunwa na kiwango cha ada iliyolipwa ili kupata bidhaa hiyo. Mapato yatokanayo na ada ya rasilimali inayovunwa katika eneo hilo yataiwezesha kamati ya maliasili kufanya kazi zake vizuri kama kununulia vifaa vya kufanyia doria, posho kwa wajumbe wa kamati pamoja na kusaidia shughuli za maendeleo ya kijiji badala ya kutegemea faini peke yake kama chanzo cha mapato. Athari za kutotenga maeneo hayo ni kwamba jamii itaendelea kukata miti yote iliyo nje ya msitu wa kijiji ili kukidhi mahitaji yao, baada ya miaka kadhaa misitu yote iliyo nje ya

eneo la hifadhi itakuwa imekwisha kabisa na hivyo watu wataanza kuvuna mazao ya misitu toka kwenye msitu wa kijiji kinyume na sheria.

Utunzaji wa takwimu mbalimbali za maliasili

Utunzaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu usimamizi wa rasilimali za misitu ni muhimu sana katika kuimarisha utawala bora katika misitu. Kamati ya maliasili ya kijiji inawajibika kutunza takwimu zote zinazohusu usimamizi wa rasilimali za misitu, endapo mwananchi au mdau mwingine wa misitu atazihitaji basi ziweze kupatikana kwa urahisi. Aina ya takwimu zinazotakiwa kuhifadhiwa ni taarifa za doria, aina ya uhalifu uliofanyika kijijini, mapato yatokanayo na ada na faini ya misitu, mihutasari ya vikao, matumizi ya mapato n.k.

Wananchi kusomewa taarifa za maliasili ya misitu

Wadau wote katika sekta ya msitu wana haki ya kupata taarifa muhimu ambazo kwa namna moja ama nyingine zinaweza kuwaathiri pindi zitakapotekelzwa. Taarifa hizi ni lazima zitolewe bure ili wananchi wote waweze kuzipata na kuzielewa. Ili kufanikisha hili lazima kijiji kiwe na utaratibu maalumu wa kuwasilisha taarifa za misitu kwa wananchi angalau mara mbili kwa mwaka.

Njia nzuri ya kuwasilisha taarifa kwa wananchi

Taarifa mbalimbali zinazohusu rasilimali ya misitu zinatakiwa kuwasilishwa kwa wananchi katika utaratibu unaohakikisha kwamba wananchi wote wanaweza kuzipata. Sehemu pekee muhimu ambayo kila mwananchi anaweza kupata taarifa husika hasa kwa wananchi waishio maeneo ya vijijini ni kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Hivyo basi taarifa zozote ni lazima ziwasilishwe kwenye mkutano mkuu wa kijiji uliohudhuriwa na idadi kubwa ya wananchi pamoja na kuzibandika taarifa hizo kwenye mbao za matangazo zilizopokijijini ili hata wale ambao hawakupata fursa ya kuhudhuria kwenye mkutano mkuu wazisome.

Maamuzi juu ya matumizi ya pesa itokanayo na misitu

Maamuzi yote yanayofanywa katika sekta ya misitu ni lazima yafanywe kwa uwazi na kwa kufuata kanuni husika. Ili kuhimiza utawala bora katika usimamizi wa misitu ni lazima kuwepo na ushiriki wa makundi yote katika jamii na wawe na sauti ya pamoja katika suala zima la kufanya maamuzi hasa yanayohusu mambo muhimu yahasusyo misitu kama matumizi ya pesa zitokanazo na misitu. Maamuzi hayo lazima yafanywe kwenye mkutano mkuu wa kijiji uliohudhuriwa na idadi inayokubalika na wananchi wapewe fursa ya kuhoji na kupatiwa majibu yaliyo sahihi.

Mgawanyo wa fedha zitokanazo na ada au faini za misitu

Ili kuhakikisha kwamba mapato yatokanayo na rasilimali za misitu kama ada na faini yanatumika kwa ufasaha, ni lazima kuwepo na utaratibu mzuri unaoanisha makundi yanayotakiwa kupata mgawanyo wa pesa hiyo na ni asilimia ngapi inatakiwa kwenda kwenye kila kundi. Mgawanyo huo lazima ulenge katika kuiwezesha kamati ya maliasili kuboresha usimamizi wa misitu na nyingine ielekezwe kwenye miradi ya maendeleo ya kijiji. Mgawanyo wa matumizi ya fedha hizo ni lazima uidhinishwe na wananchi kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Vile vile kamati ya maliasili pamoja na halmashuri ya kijiji wanawajibika kutoa taarifa ya matumizi ya fedha hizo kwenye mkutano mkuu wa kijiji.

Mikutano mkuu ya kijiji

Mkutano mkuu ni sehemu muhimu sana kwa wananchi kushiriki kufanya maamuzi au kuhakiki utekelezaji wa mambo waliyokubaliana kama vile masuala ya kifedha au kuhoji maendeleo ya shughuli za kijiji walizokubaliana. Wananchi wana haki ya kupata na kujadili taarifa mbalimbali toka kwa viongozi wao si chini ya mara 4 kwa mwaka kama ilivyoainishwa kwenye sheria za serikali za mitaa kipengele namba 8 cha 1982 na kufanyiwa mabadiliko mwaka 2002. Katika mikutano hiyo viongozi wa serikali ya kijiji wanatakiwa

kutoa taarifa zilizo sahihi na zitakazowawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za usimamizi wa misitu

Idadi ya wanawake wanaohudhuria na kuchangia mada inayoongelewa katika mkutano mkuu wa kijiji

Ushiriki wa makundi yote katika jamii husika yaani wanawake na wanaume ni muhimu na wanatakiwa kuwa na sauti sawa katika kufanya maamuzi. Hii inamaanisha kwamba makundi mbalimbali yana haki sawa ya kupata taarifa muhimu zinazohusu masuala ya misitu na zitakazowasaidia kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi yahasuyo rasilimali za misitu. Vile vile ushiriki huu lazima uambatane na uhuru wa kujieleza. Uwiano wa jinsia tofauti katika kuchangia maongezi yanayohusu misitu kwenye mkutano mkuu wa kijiji ni muhimu sana. Viongozi wa kijiji wanatakiwa kutoa nafasi/kipaumbele kwa wanawake ili waweze kuchangia katika mada zinazoongelewa kwenye mkutano mkuu badala ya kuwaachia wanaume kuongea peke yao.

Kusomwa kwa sheria ndogo kwenye mkutano mkuu wa kijiji

Katika sekta ya misitu, utawala wa kuzingatia sheria ni muhimu sana katika kusimamia rasilimali za misitu. Sheria hizi lazima zifahamike kwa wadau husika, hivyo basi wale waliopewa dhamana ya kuongoza wanatakiwa kuhakikisha kwamba wananchi wanazifahamu sheria hizo vizuri kwa njia ya kuzisoma mara kwa mara kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Uongozi wa kijiji unatakiwa kuweka utaratibu maalumu wa kuzisoma sheria ndogo za misitu kwenye mkutano mkuu wa kijiji angalau mara 2 kwa mwaka na hivyo kuongeza uelewa wa sheria kwa wananchi na kuzifuata.

Kuongezeka kwa adhabu pindi mhalifu arudiapo kosa

Ili kuweza kudhibiti uhalifu wa misitu, ni lazima kuwepo na mabadiliko katika utolewaji wa faini kwa mhalifu. Adhabu/faini itolewayo kwa ajili ya kosa dogo lazima iwe ni ndogo ili kumuwezesha mhalifu kulipa faini hiyo kwa urahisi. Endapo mhalifu atavunja sheria hiyo kwa mara ya pili adhabu yake lazima iongezeke na iendeleo kuongezeka mara idadi ya makosa anayofanya. Vile vile ni lazima kuwepo na utofauti kati ya faini ya kosa dogo na kubwa, mtu akifanya kosa kubwa basi faini yake iwe kubwa tofauti na yule aliyetenda kosa dogo na yenyewe iongezeke pindi mhalifu anaporudia kufanya kosa hilo. Utaratibu huu wa faini unawakatisha tamaa watu kuendelea kufanya uhalifu wa misitu kwani mapato yapatikanayo kutokana na uvunaji haramu wa misitu yatakuwa yanaishia kulipia faini na hivyo kushindwa kufaidika na shughuli hiyo. Faini zote hizo na adhabu nyingine ni lazima zifafanuliwe vizuri kwenye sheria ndogo za usimamizi wa misitu na sheria hizo zitumike kuadhibu wahalifu.

Ushiriki wa wananchi katika kuchagua mjumbe wa kamati ya maliasili ili kuziba nafasi

Ushiriki wa wananchi katika kuchagua wajumbe wa kamati ya maliasili huwapa nguvu wananchi ya kuwawajibisha wanakamati waliowapa jukumu la kuwaongoza kwa matokeo mabaya ya uongozi wao. Inapotokea kwamba kuna nafasi iliyo wazi kwenye kamati ya maliasili inailazimu serikali ya kijiji kuitisha mkutano mkuu wa dharura utakaotoa fursa kwa wananchi kuchagua mtu mwingine wanayeona anafaa kuziba nafasi hiyo. Vile vile utaratibu huu utaisaidia kamati kuweza kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangwa kuliko kusubiri mpaka uchaguzi mwingine utavyotokea ndipo waweze kupata watu wa kuziba nafasi hizo.

Taratibu za kukosoa utendaji kazi wa wajumbe wa kamati ya maliasili

Wananchi wana jukumu la kuhakikisha kwamba wajumbe wa kamati ya maliasili wanatekeleza majukumu waliyopangiwa basi wananchi wana wajibu wa kutoa maoni yao kwa njia ya kuhudhuria kwenye mkutano mkuu wa kijiji na kutoa maoni yao au kwa kutoa maoni yao kwenye sanduku la maoni la kijiji kuhusu utendaji mbovu wa wanakamati na maamuzi ya kuwawajibisha yatatolewa. Maoni yanayowekwa kwenye

sanduku yatatakiwa kufanyiwa kazi vizuri na kwa wakati na malalamiko yaliyotolewa yafikishwe kwenye mkutano mkuu wa kijiji ili yaweze kufanyiwa maamuzi na wananchi.

Utaratibu wa kupitia mpango wa usimamizi wa misitu

Ili kuweza kuimarisha usimamizi wa misitu ya kijiji ni lazima kuwepo na utaratibu wa kuupitia mpango wa usimamizi wa misitu. Hii itawasaidia wananchi kubadilisha mambo yanayopelekea uharibifu wa msitu kuendelea na kuongeza mambo yanayotakiwa kuwemo kwenye mpango ili kuboresha msitu wa kijiji. Mpango upitiwe angalau kila baada ya miaka mitatu.

Upatikanaji wa mpango wa usimamizi wa msitu na sheria ndogo za misitu.

Ili jamii iweze kushiriki kikamilifu katika kusimamia rasilimali za misitu inawajibika kushiriki kikamilifu katika kutunga sheria ndogo za usimamizi wa misitu na kuandaa mpango wa usimamizi wa misitu na kuutekeleza. Nakala za sheria ndogo pamoja na mpango wa usimamizi wa msitu zinatakiwa ziwe wazi kwa wananchi na kwa wadau wengine wa misitu. Nakala hizo zinatakiwa ziwekwe kwenye ofisi ya serikali ya kijiji na kwenye uongozi wa kamati ya maliasili na ziweze kupatikana pale zinapohitajika.

Mipaka katika msitu wa hifadhi wa kijiji

Ili wananchi waweze kusimamia na kulinda msitu wao vizuri, ni muhimu kwa kila kijiji kufahamu vizuri mipaka ya eneo lake la msitu. Msitu huo unatakiwa kuwekewa mipaka inayoonekana kwa urahisi kwa kila mtu kama vizuizi vya moto, kuchora ramani au kupanda miti. Kila mwananchi ana jukumu la kuiheshimu na kulinda mipaka hiyo dhidi ya wahalibifu wa misitu.